

HALMASHAURI YA WILAYA YA MUHEZA



TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza anawatangazia wananchi wote wenye sifa kuomba nafasi za kazi kama ifuatavyo;

1. KATIBU MUHSUSI DARAJA III - (NAFASI 2)

(i) Sifa za kuingilia kazini.

(a) Kuajiriwa wahitimu wa Kidato cha IV waliohudhuria mafunzo ya Uhazili na kufaulu mtihani wa hatua ya tatu, wawe wamefaulu somo la Hatimkato ya Kiswahili na Kiingereza maneno 80 kwa dakika moja, wawe wamepata mafunzo ya Kompyuta kutoka Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali na kupata cheti katika Programu za Windows ,Microsoft Office, Internet, Email na Publisher.

(b) Awe na umri usiozidi miaka 45.

(ii) Kazi za kufanya.

- (i). Kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida
- (ii). Kupokea wageni na kuwasaili shida zao na kuwaelekeza sehemu wanayoweza kushughulikiwa.
- (iii). Kusaidia kutunza taarifa/ kumbukumbu za matukio, miradi, wageni, tarehe za vikao, Safari za mkuu wake na ratiba za kazi zingine zilizopangwa kutekelezwa katika Ofisi anamofanya kazi na kumuarifu Mkuu wake kwa wakati unaohitajika.
- (iv). Kusaidia kutafuta na kumpatia Mkuu wake majalada, nyaraka au kitu chochote kinachoohitajika katika shughuli za kazi hapo Ofisini.
- (v). Kusaidia kufikisha maelezo ya Mkuu wake wa kazi kwa wasaidizi wake na pia kunuarifu kuhusu taarifa zozote anazokuwa amepewa na wasaidizi hao.
- (vi).Kusaidia kupokea majalada , kuyagawa kwa Maofisa walio katika sehemu alipo, na kuyakusanya, kuyatunza na kuyaarudisha sehemu zinazohusika.
- (vii).Kutekeleza kazi zozote ataakazokuwa amepangiwa na Msimamizi wake wa kazi.

(iii) Ngazi ya Mshahara

Ngazi ya Mshahara kwa cheo hiki ni TGS.B.1 yaani Mshaaharaa wa Tshs.**390,000/=** kwa mwezi

2. MTENDAJI WA KIJIJI III (NAFASI 2)

(i) Sifa za kuingilia kazini

(a) Kuajiriwa wenye elimu ya kidato cha nne (IV au VI) aliyejiitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti katika moja ya Fani zifuataazo: Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kina chotambuliwa na Serikali

(b) Awe na umri usiozidi miaka 45

(ii) Kazi na majukumu ya Mtendaji wa Kijiji III

- (i). Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
- (ii).Kusimamia ulinzi na Usalama wa Raia na mali zao, kuwa mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji
- (iii).Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya kijiji
- (iv).Katibu wa mikutano na kamati zote za Halmashauri ya kijiji

- (v).Kutafsiri na kusimamia serea, sheria na taratibu.
- (vi).Kuandaa Taarifa za utekelezaji na kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuanda na kutekeleza mikakati kuondoa njaa,umaskini na kuongeza uzalishaji mali.
- (vii).Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya kitaalam katika Kijiji
- (viii).Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji
- (ix).Mwenyekiti wa Kikao cha wataalam waliopo katika Kijiji.
- (x).Kupokea kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi.
- (xi).Kusimamia utungaji wa Sheria ndogo za kijiji na
- (xi).Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata

(iii) Ngazi ya Mshahara

Ngazi ya Mshahara kwa cheo hiki ni TGS.B.1 yaani Mshahara wa Tshs.**390,000/=** kwa mwezi

3. DEREVA DARAJA II (NAFASI 2)

(i) Sifa za kuingilia kazini

- (a)Kuajiriwa wenyе cheti cha mtihani wa kidato cha IV, wenyе Leseni daraja “C”ya uendeshaji pamoja na uzoefu wa kuendesha magari kwa muda usiopungua miaka mitatu bila ya kusababisha ajali, wenyе cheti cha majaribio ya ufundi Daraja la II.

- (b).Awe na umri usiozidi miaka 45

(ii) Kazi na majukumu

- (i).Kuhakikisha gari na vyombo vyake vipo katika hali ya nzuri wakati wote, na kufanya ukaguzi wa gari kabla na baada ya safari ili kugundua ubovu unaohitaji matengenezo.
- (ii).Kufanya matengenezo madogo madogo katika gari.
- (iii).Kutunza na kuandika daftari la safari “Log book” kwa safari zote

(iii) Ngazi ya Mshahara

Ngazi ya Mshahara kwa cheo hiki ni TGOS.A.1 yaani Mshahara wa Tshs.**300,000/=** kwa mwezi

MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI

- (a).Maombi yote yaambatanishwe na vivuli vya vyeti vya kumaliza shule na mafunzo.
- (b).Maombi yote yaambatanishwe na maelezo binafsi ya mwombaji (CV) na wadhamini wawili na namba zao za simu.
- (c).Waombaji wote wanatakiwa kuwa na vyeti vya kuzaliwa
- (d).Maombi yawe na anuani kamili pamoja na namba za simu ili kurahisisha mawasiliano.
- (e).Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 04/09/2017 Saa 9.30 alasiri
- (f).Waombaji wenyе sifa wataitwa kwenye usaili.
- (g) Kwa waombaji waliokuwa kazini maombi yao **LAZIMA** yapitie kwa Waajiri wao.
- (h).Maombi yote yatumwe kwa

MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA

HALMASHAURI YA WILAYA

S.L.P 20

MUHEZA

Luiza O.Mlelwa
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
MUHEZA